# UCHAGUZI

Jarida la Tume ya Taifa ya Uchaguzi Toleo Na. 17 Novemba, 2023

TOLEO MAALUM

HALIUZWI




'Wadau wa uchaguzi ni muhimu katika kufanikisha uboreshaji wa Daftari'
**Uk.03**

Kishkwambi, Simu Janja kurahisisha Uandikishaji Wapiga Kura.
**Uk.06**

NEC yaridhishwa na Mwitikio wa Wananchi katika Uandikishaji wa Majaribio.
**Uk.08**

Ifahamu Tume

# Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura limeanzishwa chini ya Ibara ya 5(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 12(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 na Kifungu cha 15B(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

Tangu kuanzishwa kwa Tume, Daftari la Kudumu la Wapiga Kura limetumika kwa mara ya kwanza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

Kwa mujibu wa Ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na mambo mengine inawajibika:-

(i) Kusimamia na kuratibu Uandikishaji wa Wapiga Kura wapya waliotimiza umri wa kuandikishwa; na

(ii) Kusimamia na kuratibu Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

**•Wajibu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 15 (5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 21 (5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina wajibu wa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili, baada ya Uchaguzi Mkuu uliomalizika na kabla Uchaguzi Mkuu mwingine unaofuatia.

**•Sifa za Kuandikishwa Kuwa Mpiga Kura**

Kwa mujibu wa Ibara ya 5(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 10 (1) na (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 15(1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, sifa za mtu kuandikishwa kuwa Mpiga Kura ni:-

(i) Awe Raia wa Tanzania;

(ii) Awe ametimiza umri wa miaka 18; na

(iii) Awe hajapoteza sifa kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi au Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge.




# ‘Wadau wa uchaguzi ni muhimu katika kufanikisha uboreshaji wa Daftari’

***Na Mwandishi wetu***

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imesema inatambua mchango mkubwa unaotolewa na wadau wa uchaguzi katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na ushirikiano katika kutoa elimu ya mpiga kura.

Akifungua mkutano wa wadau wa uchaguzi uliofanyika tarehe 17 Novemba, 2023 jijini Dar es salaam ambao ni Viongozi wa Dini, Asasi za kiraia, Wahariri wa vyombo vya habari, Watu wenye ulemavu, Wanawake na Vijana kuhusu uboreshaji wa majaribio wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji (Rufaa) Mhe. Jacobs Mwambegele amesema wadau hao wana mchango mkubwa katika kudumisha demokrasia, upendo, amani na utulivu nchini.

“Kwa kuzingatia hilo, Tume imekuwa ikikutana nanyi kwa ajili ya kuwapa taarifa katika vipindi vya maandalizi ya kazi zake, kujadiliana kwa pamoja na kupokea ushauri na maoni mbalimbali kutoka kwenu lengo likiwa ni kuimarisha ushirikiano na kuongeza ufanisi wa Tume,” amesema Jaji. Mwambegele.

Jaji Mwambegele amewajulisha wadau hao kuwa lengo la




uboreshaji wa majaribio ni kupima uwezo wa vifaa na mifumo itakayotumika wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura unaotarajiwa kufanyika nchi nzima kwa tarehe zitakazopangwa na kutangazwa na Tume.

Uboreshaji wa Majaribio ulifanyika kuanzia tarehe 24 hadi 30 Novemba, 2023 katika Kata ya Ng'ambo iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Mkoa wa Tabora na Ikoma iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, Mkoa wa Mara ambapo vituo 16 vya kuandikisha wapiga kura vilitumika.

Vituo hivyo vilifunguliwa saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni na kati ya hivyo, vituo 10 ni vya kata ya Ng'ambo na sita (6) ni vya kata ya Ikoma.

Uboreshaji huo ulihusisha kuandikisha raia wa Tanzania wenye umri wa miaka 18 au zaidi au raia ambao watatimiza umri wa miaka 18 kabla au ifikapo tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Kundi lingine lililohusika kwenye zoezi hilo ni pamoja na wapiga kura waliohitaji kuboresha taarifa zao na ambao walihama kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda eneo lingine, waliopoteza au kadi zilizoharibika, waliohitaji kurekebisha taarifa zao na kuondoa wapiga kura waliopoteza sifa za kuwemo katika Daftari.

Tahariri

# Hongereni Wadau wa Uchaguzi kufanikisha Uboreshaji wa Majaribio

Tarehe 10 Novemba 2023, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitangaza kufanyika kwa zoezi la Uboreshaji wa Majaribio katika kata za Ng'ambo katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na kata ya Ikoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya katika Mkoa wa Mara, zoezi ambalo lilipangwa kufanyika kuanzia tarehe 24 hadi 30 Novemba, 2023.

Ingawa lengo la uboreshaji wa majaribio lilikuwa ni kuangalia uwezo na ufanisi wa vifaa na Mfumo wa Uandikishaji Wapiga Kura ili kubaini mapungufu ambayo yanaweza kujitokeza kabla ya kuanza kwa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura litakalohusisha nchi nzima kwa tarehe na ratiba itakayopangwa na Tume, hakuna shaka yoyote tunaweza kusema kuwa zoezi la uboreshaji wa majaribio lilifanikiwa.

Dalili za kufanikiwa kwa zoezi hili zilianza kujitokeza tangu siku ambayo Mkurugenzi wa Uchaguzi Bw. Kailima Ramadhani alitangaza tarehe za kufanyika kwa zoezi hili ambapo wadau wa uchaguzi wakiwemo waandishi wa habari waliweza kutoa ushirikiano kwa Tume kupitia vyombo vyao kwa kuhakikisha wananchi wanapata taarifa kuhusu kufanyika kwa zoezi hilo.

Kadhalika katika Mikutano ya Wadau ambayo Tume iliifanya kwa wadau mbalimbali wa uchaguzi hususani ule wa vyama vya siasa, Viongozi wa Tume wakiongozwa na Mwenyekiti wa Tume Jaji (Rufaa) Mhe. Jacobs Mwambegele walisisitiza umuhimu wa wadau wote wa uchaguzi kuhamasisha umma na kushiriki kwenye zoezi la kujiandikisha na kuboresha taarifa zao kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mbali na kuitisha mikutano miwili ya wadau iliyofanyika jijini Dar es salaam, Tume ilifanyika mikutano mingine miwili ya wadau wa uchaguzi katika mikoa ya Tabora na Mara kwa lengo hilo hilo la kuwashirikisha wadau ili waweze kuwahamasisha wananchi kushiriki kwenye zoezi la uboreshaji wa majaribio
.

Tunapenda kutoa pongezi zetu kwa maelfu ya wakazi wa kata za Ng'ambo katika halmashauri ya Manispaa ya Tabora katika mkoa wa Tabora na Ikoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya katika mkoa wa Mara ambao waliweza kujitokeza kwa wingi kujiandikisha na kuboresha taarifa zao katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Kutokana na kufanikiwa kwa zoezi hilo tunasema heko kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kufanikisha hatua hiyo muhimu lakini pia tunatoa pongezi nyingi kwa wadau wote wa uchaguzi kwa kuhakikisha kuwa malengo ya kufanyika kwa zoezi hili yanafanikiwa.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaamini kuwa wadau wote wa uchaguzi watadumisha ushirikiano huu ili pale kipenga cha kuanza kwa zoezi lenyewe la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kitakapopulizwa wananchi wajitokeze maradufu kujiandikisha na kuboresha taarifa zao.

Kadhalika Tume inavipongeza vyama vyote vya siasa ambavyo vilijitokeza kuweka mawakala katika vituo vya kujiandikisha kwani tunaamini kuwa mawakala hawa siyo tu walikuwa na jukumu la kushuhudia na kujiridhisha kuhusu taratibu zinazotumika wakati wa uboreshaji wa majaribio wa Daftari lakini pia walitoa hamasa kubwa kwa wanachama wa vyama vyao kujitokeza kushiriki kwenye zoezi hili.

Aidha, tunapenda kutoa pongezi zetu za dhati kwa vyombo vya habari ambavyo viliweza kuuhabarisha umma kuhusu kufanyika kwa zoezi hilo, na pia kutoa fursa kwa maafisa wa Tume kuzungumza na wananchi kupitia vyombo hivyo ili kutoa elimu ya mpiga kura.



# Kishkwambi, Simu Janja kurahisisha Uandikishaji Wapiga Kura

***Na Mwandishi wetu***

Tume ya Taifa ya uchaguzi (NEC) imeeleza kuwa matumizi ya kishkwambi chenye uwezo wa kubeba taarifa zote za wapiga kura yamerahisisha uandikishaji wa wapiga kura katika zoezi la uboreshaji wa majaribio wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika kata za Ng'ambo na Ikoma kulinganisha na matumizi ya BVR kubwa iliyokuwa ikiunganishwa na kompyuta hapo awali kwani ilikuwa na uwezo wa kubeba taarifa za wapiga kura pekee.

Hayo yamebainishwa na Afisa TEHAMA Mkuu kutoka Tume ya Taifa ya uchaguzi (NEC) Bw. Lazaro Madembwe, wakati akielezea mifumo ya TEHAMA ya BVR na OVRS katika Kituo cha Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Shule ya Sekondari ya wasichana Tabora iliyopo Kata ya Ng'ambo Mkoani Tabora.

Amesema kifaa cha kishkwambi kinachotumika sasa kina kamera yenye uwezo kupiga picha na kuchukua taarifa zote za mpiga kura zikiwemo, alama za vidole, saini na kuhifadhi viambatanisho mbalimbali vya mpiga kura na hivyo kurahisisha uandikishaji wa wapiga kura kulinganisha na teknolojia iliyokuwa ikitumika huko nyuma ambayo ilihusisha matumizi ya BVR kubwa iliyounganishwa na kompyuta.

Bw. Madembwe amefafanua kuwa katika uboreshaji wa majaribio Tume imetumia teknolojia ya (Biometric) kuandikisha wapiga kura,ambapo kupitia kifaa cha kishkwambi kina uwezo wa kuchukua alama za vidole ili kuweza kuwatambua wapiga kura walioandikishwa zaidi ya mara moja

na kuondoa taarifa za waliojirudia ambazo ziko kwenye daftari.

"Teknolojia hii ilitumika kwa mara ya kwanza kwa uandikishaji mwaka 2015 na uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura mwaka 2019 na 2020 na vifaa vilivyotumika ilikuwa ni BVR ambayo ilikuwa na Laptop na kamera ambavyo vilikuwa vinakaa tofauti tofauti lakini kuelekea uboreshaji unaofanyika sasa vifaa vyote vinakaa kwenye Kishkwambi ambapo unaskani Nyaraka na kupiga picha kwa kutumia kishikwambi," amesema Madembwe.

Ameongeza kuwa Tume imejitahidi sana kupanua wigo wa huduma hapo awali mpiga kura ilikuwa ni lazima afike kituoni kwa ajili ya kuboresha taarifa zake, lakini hivi sasa mpiga kura anaweza kuanzisha mchakato wa awali wa kuboresha taarifa zake kupitia kwenye simu janja au kompyuta iliyounganishwa na intaneti na baada ya hapo atapokea ujumbe mfupi wenye kumbukumbu namba ukimtaka kufika kituoni kwa ajili ya kukamilisha taarifa zake.

“Mfumo huu unaendeshwa kwenye programu wezeshi ambayo ni (Android) ukilinganisha na mwaka 2015,2019 na 2020 ambapo programu hiyo ilikuwa inaendeshwa na (Windows) , programu ya Sasa ni nyepesi na ina uwezo wa kuchakata taarifa za wapiga kura kwa haraka zaidi,” amefafanua.

Bw.Madembwe amesisitiza kuwa vifaa vya sasa vinavyotumika kwenye uandikishaji vina uzito mdogo wa kilo 15 ukilinganisha na vya awali ambavyo vilikuwa na uzito wa kilo 35, hivyo vinabebeka kwa urahisi na vinarahisisha shughuli za usafirishaji.

"Walengwa wa zoezi hili ni watanzania wote walioandikishwa hapo awali ambao wamehama kata, waliopoteza au kadi zao kuharibika na wale wote wanaotaka kuboresha taarifa zao,” amesema Bw.Madembwe na kuongeza:

“Wananchi wanaolengwa katika zoezi hili ni wale wenye sifa ya kuandikishwa kuwa wapiga kura na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na pia zoezi hili litawahusu wananchi ambao  wametimiza umri wa miaka 18 au watatimiza miaka 18 ifikapo siku ya uchaguzi mkuu 2025.”

Bw. Madembwe amesisitiza kuwa mfumo huo umeboreshwa na una uwezo wa kudhibiti waombaji wote ambao watataka kuandikishwa wakati hawajafikisha umri wa miaka 18 hivyo ametoa wito kwa wananchi wote wenye sifa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha.

Aidha, Afisa huyo wa Tume ameeleza kuwa Tume imekuja na njia mpya ya uboreshaji kwa mtandao, mfumo unaomuwezesha mpiga kura kuanzisha mchakato wa kuboresha taarifa zake kwenye mtandao.

“Mpiga kura anayetaka kuboresha taarifa zake kwa njia ya mtandao atalazimika kuingia kwenye tovuti ya Tume www.nec.go.tz na kubonyeza kiunganishi kilichoandikwa boresha taarifa za mpiga kura au atatumia anuani ya ovrs.nec.go.tz na atafuata maelekezo yaliyowekwa ili kujaza taarifa zake kwa njia ya mtandao,” anaeleza.



# NEC yaridhishwa na Mwitikio wa Wananchi katika Uboreshaji wa Majaribio

***Na Mwandishi wetu***

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imesema zoezi la uboreshaji wa majaribio wa daftari la kudumu la mpiga kura katika Kata za Ikoma iliyoko wilayani Rorya mkoani Mara na Kata ya Ng'ambo iliyoko Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Mkoa wa Tabora linaendelea vizuri, huku kukiwa na mwitikio mkubwa wa watu.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Idara ya Daftari na TEHAMA kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi Bw. Geofrey Mpangala akiwa katika kituo cha kuandikisha wapiga kura cha Masempele katika Kata ya Ng'ambo, wakati akizungumzia kuhusu mwitikio wa wananchi katika kushiriki zoezi la uboreshaji wa majaribio wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambao umefanyika kuanzia Novemba 24-30 mwaka huu.

Amesema mwitikio wa wananchi umekuwa mkubwa kwani wamejitokeza kwa idadi kubwa ili kujiandikisha na wapiga kura wamepata nafasi ya kuboresha taarifa zao katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Aidha ameongeza kuwa wananchi wa Kata za Ng'ambo katika Manispaa ya Tabora na Ikoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya wana fursa ya kuzitumia siku saba zilizowekwa na Tume ambazo ni kuanzia tarehe 24 hadi 30 Novemba, 2023 kwa ajili ya kujiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga kura.

Amefafanua kuwa wananchi wana fursa ya kujiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kufika katika vituo vya kujiandikisha ambavyo vimeainishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambapo watapata fursa ya kuandikishwa moja kwa moja au pia kutumia njia ya mtandao kuboresha taarifa zao.

"Tunao mfumo wa kuboresha taarifa za wapiga kura kwa njia ya mtandao (OVRS ) Lakini mpaka sasa hakuna aliyeboresha taarifa hizo kwa njia hiyo, hivyo, kuna kila sababu ya kuelimisha zaidi wananchi ili wauelewe zaidi mfumo huo wa kuboresha taarifa zao kwa njia ya mtandao na waweze kuutumia," amesisitiza Bw. Mpangala.

Naye msimamizi wa kituo cha Masempele katika Kata ya Ng'ambo, Bi. Mwatano Juma, amesema kuwa zoezi linaendelea vizurikatika kituo chake kwani wapiga kura wote wanaofika katika Kituo hicho wanafuata taratibu zote za uandikishaji kwa kutoa taarifa zao muhimu kwa ajili ya kuandikishwa au kuboresha taarifa zao.

Bw. Simon Mlimanazi ambaye ni mpiga kura mmojawapo aliyefika katika Kituo cha Kizigo kwa ajili ya kujiandikisha, amesema kuwa zoezi linaendelea vizuri kwani katika kituo hicho amepata huduma kwa wakati na amekamilisha taratibu zote hatimaye amekabidhiwa kadi yake ya mpiga kura.





# 'Wekeni utaratibu kuviwezesha vyama vya siasa kushiriki uboreshaji'

**Na Mwandishi wetu**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imewataka Watendaji wa Uchaguzi walioshiriki zoezi la Uboreshaji wa Majaribio ambalo lilifanyika katika kata mbili za Halmashauri ya Wilaya ya Rorya na Manispaa ya Tabora kuandaa utaratibu mzuri ambao utatoa fursa kwa vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi kushiriki katika zoezi hilo.

Akifungua mafunzo kwa watendaji wa uchaguzi yaliyofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya kabla ya kuanza kwa zoezi hilo, Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Jaji wa Rufaa Mhe. Mwanaisha Kwariko alisema kuwa vyama vya siasa viliruhusiwa kuweka mawakala katika uboreshaji huo.

Mjumbe huyo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi aliwafahamisha watendaji hao kuwa vyama vya siasa viliruhusiwa kuweka mawakala katika vituo vya uandikishaji katika kipindi chote cha zoezi la uboreshaji wa majaribio kilipokuwa kikifanyika.

Aliwataka watendaji hao kuvishirikisha vyama vya siasa katika masuala yote ambayo walistahili kushirikishwa ili

watekeleze majukumu yao kwa ufanisi na kuwasisitiza kuweka utaratibu mzuri ili kuviwezesha vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi kushiriki kikamilifu katika zoezi hilo.

Jaji Kwariko alitoa wito kwa watendaji hao kuhakikisha kuwa wanafanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Maelekezo ya watakayopewa na Tume.

Naye Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Mhe. Dkt. Zakia Mohamed Abubakar ambaye alifungua mafunzo kama hayo kwa watendaji wa uchaguzi katika Manispaa ya Tabora aliwataka watendaji wa uchaguzi kuhakikisha kuwa wanasimamia na kutunza vifaa vilivyokusudiwa kutumika katika zoezi hilo.

"Hakikisheni kuwa mnasimamia utunzaji wa vifaa vyote vya uboreshaji wa majaribio kwani vimenunuliwa kwa gharama kubwa," ameeleza Mhe. Dkt. Zakia.

Mafunzo kwa watendaji wa uchaguzi yaliwajumuisha Mratibu wa Uandikishaji wa Uchaguzi wa Mkoa, Afisa Mwandikishaji wa Jimbo, maafisa waandikishaji wasaidizi, maafisa ugavi, maafisa TEHAMA na maafisa wanaoshughulikia masuala ya uchaguzi katika kata hizo mbili.





# Mitandao ya Simu kutumika kwenye Uboreshaji

***Na Mwandishi wetu***

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imesema wapiga kura walioshiriki katika zoezi la uboreshaji wa majaribio lililofanyika kuanzia tarehe 24 hadi 30 Novemba, 2023 katika Kata ya Ng'ambo iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na Ikoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya walikuwa na fursa ya kuboresha taarifa zao kwa njia ya mtandao kwa kutumia simu zao za mkononi au kompyuta.

Mkurugenzi wa Uchaguzi Bw. Kailima Ramadhani amesema kuwa utaratibu wa kuboresha taarifa kwa njia ya mtandao, hautawahusu wapiga kura wanaotaka kuandikishwa kwa mara ya kwanza na wapiga kura ambao kadi zao zimeharibika au kupotea.

"Hawa wanashauriwa wafike kwenye kituo cha kuandikisha wapiga kura na kufuata taratibu watakazoelekezwa na Maafisa wa Tume watakaokuwepo kwenye kituo," amesisitiza Bw.Kailima

Bw. Kailima ameeleza kuwa utaratibu wa kuboresha taarifa kwa njia ya mtandao utamhusu mpiga kura ambao ameandikishwa kwenye Daftari

la Kudumu la Wapiga Kura na anahitaji kuanzisha mchakato wa kuboresha taarifa zake ama kwa kubadilisha kituo cha kupigia kura iwapo amehama Mkoa au Wilaya nyingine au kurekebisha taarifa zake.

“Mfumo wa uandikishaji ulioboreshwa utawawezesha wapiga kura ambao wameshaandikishwa na wapo kwenye daftari la wapiga kura kuanzisha mchakato wa kuboresha taarifa zao ama kwa kubadilisha kituo cha kupigia kura iwapo amehama Mkoa au Wilaya nyingine au kurekebisha taarifa zao kwa njia ya mtandao kwa kutumia simu zao za mkononi au kompyuta,” amesisitiza Bw. Kailima na kuongeza:

“Kuanzisha mchakato mtandaoni, mpiga kura ataingia kwenye tovuti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo ni www.nec.go.tz kwa kutumia kompyuta au simu janja kisha atabonyeza kiunganishi kilichoandikwa ‘Boresha Taarifa za Mpiga Kura’ au atatumia anuani ya *ovrs.nec.go.tz* itakayompeleka moja kwa moja kuanzisha mchakato.”




Uboreshaji wa majaribio ulifanyika kuanzia tarehe 24 hadi 30 Novemba, 2023 na katika vituo 16 ambapo vituo 10 ni vya kata ya Ng’ambo na vituo sita (6) vipo kata ya Ikoma.

Vituo vya uandikishaji vilifunguliwa saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni ambapo zoezi hilo limefanyika kwa lengo la kupima uwezo wa vifaa na mifumo ya uandikishaji itakayotumika wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura unaotarajiwa kufanyika nchi nzima kwa tarehe na ratiba itakayopangwa na Tume.




# NEC yakutana na Vyama vya siasa

***Na Mwandishi wetu***

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekutana na Viongozi kutoka Vyama vya siasa ili kuwahimiza kushiriki kwenye zoezi la uboreshaji wa majaribio wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambalo limefanyika kuanzia tarehe 24 hadi 30 Novemba, 2023 katika Kata za Ng'ambo katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Mkoa wa Tabora na Ikoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, Mkoa wa Mara.

Akifungua mkutano wa Tume na vyama vya siasa ambao ulifanyika jijini Dar es Salaam, mnamo tarehe 16 Novemba, 2023, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji (Rufaa) Mhe. Jacobs Mwambegele amesema Vyama vya siasa viliruhusiwa kuweka wakala mmoja katika kila kituo cha kuandikisha wapiga kura.

"Lengo ni kushuhudia na kujiridhisha juu ya taratibu zilizopangwa kutumika wakati wa uboreshaji wa majaribio," amesema Jaji Mwambegele.

Uboreshaji wa majaribio ulilenga kupima uwezo wa vifaa na mifumo itakayotumika wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura unaotarajiwa kufanyika nchi nzima

kwa tarehe zitakazopangwa na kutangazwa na Tume.









# Wadau wa Uchaguzi wahimizwa kuhamasisha wananchi kushiriki uboreshaji

***Na Mwandishi wetu***

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imesema wadau wa uchaguzi wana jukumu la kufikisha ujumbe sahihi kwa wananchi ambao utawawezesha walio na sifa ya kuandikishwa na kuboresha taarifa zao kujitokeza kwa wingi kushiriki zoezi la uboreshaji wa majaribio wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lililofanyika kuanzia tarehe 24 hadi 30 Novemba, 2023.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Bw. Kailima Ramadhani ameyasema hayo tarehe 20 Novemba, 2023 wakati akifungua mkutano wa Tume na wadau wa uchaguzi uliofanyika kwenye ukumbi wa Hoteli ya Mapsap Linme katika wilaya ya Rorya mkoani Mara.

Aliwaasa wadau hao kuendelea kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo katika kipindi chote cha uboreshaji wa majaribio wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.
Pia, aliwaasa kuendelea kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo katika kipindi




chote cha uboreshaji wa majaribio la Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Aidha, Mkurugenzi wa Uchaguzi alisema kuwa Tume imehakikisha kuwa wananchi wamepata uelewa wa kutosha kuhusu uboreshaji wa majaribio kwa kutumia njia mbalimbali za kutoa elimu ya mpiga kura zikiwemo kukutana na wadau wengine wa uchaguzi.

Aliongeza kuwa katika zoezi la uboreshaji wa majaribio, vyama vya siasa viliruhusiwa kuweka wakala mmoja katika kila kituo cha kuandikisha wapiga kura, lengo ni kushuhudia na kujiridhisha juu ya taratibu zilizopangwa kutumika.

Mkutano wa wadau wa uchaguzi uliwashirikisha viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini, wazee wa kimila, watu wenye ulemavu, wawakilishi wa vijana, wawakilishi wa wanawake na asasi za kiraia kwa ujumla kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Rorya.



# Wajumbe NEC waridhishwa na Uboreshaji wa Majaribio Kata ya Ikoma

***Na Mwandishi wetu***

Baadhi ya Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ambao wameshiriki kutazama zoezi la Uboreshaji wa majaribio wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Kata ya Ikoma iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Rorya Mkoani Mara wameelezea kuridhishwa kwao na mwitikio wa wananchi ambapo kufikia tarehe 28 Novemba, 2023, ikiwa ni siku nne tangu zoezi hilo kuanza jumla ya Wapiga Kura 1,613 wamejitokeza kujiandikisha katika kata hiyo.

Mmoja wa Wajumbe hao ambaye ni Jaji wa Mahakama Kuu Mhe. Asina Omar amesema mwitikio wa wananchi katika kujiandikisha na kuboresha taarifa zao ni mkubwa na mawakala wameshiriki kikamilifu katika zoezi hilo ikiwa ni pamoja na kuwabaini wananchi waliopoteza sifa za kuwa Wapiga Kura ili taarifa zao ziondolewe katika Daftari la Kudumu la Wapiga kura.

“Zoezi linakwenda vizuri, tumeshuhudia katika vituo tulivyotembelea hakuna changamoto na zilizopo zimetatuliwa na wataalam kwa kushirikiana na mawakala wa vyama waliopo vituoni jambo ambalo linaonesha lengo la zoezi hili kutimia kama ilivyokusudiwa,”

amesema Jaji Asina.

Amesema, muda unaotumika kuandikisha au kuboresha taarifa za Mpiga Kura unazidi kuwa mfupi na kuimarika kwa huduma vituoni kadri zoezi hilo linavyoendelea na hivyo kuleta ufanisi zaidi siku hadi siku na kuonesha uwezo wa vifaa vinavyotumika.

Kwa upande wake Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Magdalena Rwebangira amesema ameridhishwa namna zoezi linavyofanyika hivyo lengo la zoezi hilo la kufanyia majaribio vifaa vya uboreshaji pamoja na mifumo ya uboreshaji wa Daftari linatimia kwani changamoto zinabainika na kutatuliwa mapema.

Katika ziara hiyo Jaji Asina aliambatana na Mhe. Mwanaisha Kwariko ambaye ni Jaji wa Mahakama ya Rufaa na Mhe. Magdalena Rwebangira ambao wametembelea vituo mbalimbali vya uandikishaji wapiga kura katika Kata ya Ikoma na kushuhudia jinsi zoezi hilo la uboreshaji wa majaribio linavyofanyika.

Akitoa taarifa ya siku nne za uboreshaji wa majaribio katika Kata ya Ikoma, Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi, Bw. Grayson Orcado kwa niaba ya Mkurugenzi wa Uchaguzi amesema, zoezi hilo linakwenda vizuri na kwa ufanisi mkubwa kwani hadi wakati huo jumla ya wananchi 1,613 wamejitokeza vituoni ambapo kati ya hao 1,356 wamejiandikisha kuwa wapiga kura na wapiga kura 257 wameboresha taarifa zao.

Amesema, mawakala wa vyama wanaonesha ushirikiano wa hali ya juu hasa katika changamoto za utambuzi wa wakazi wa maeneo yao kwa kuzingatia kuwa Kata ya Ikoma ina mwingiliano wa raia wa nchi jirani.

Ushirikiano baina ya mawakala hao kutoka vyama mbalimbali vya siasa uliwezesha kuwabaini watu wanane ambao siyo raia wa Tanzania waliotaka kujiandikisha kuwa wapiga kura katika kituo cha kujiandikisha wapiga kura cha Shule ya Msingi Nyamasanda, Bw. Silvanus Owan’ge ambaye ni Wakala wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) katika Kituo cha Ofisi ya Mtendaji Kata ya Ikoma ameelezea, kuridhishwa kwake na namna zoezi hilo lilivyo la uwazi na kupongeza Tume kwa namna inavyofanya kazi kwa kushirikiana nao.



# 'Jitokezeni kujiandikisha uboreshaji wa majaribio'

***Na Mwandishi wetu***

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imewaasa wakazi wa maeneo yaliyoteuliwa kwa ajili ya uboreshaji wa majaribio wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kujitokeza kwa wingi kushiriki kwenye zoezi hilo ambalo linalenga kupima utayari wa mifumo na vifaa vya uboreshaji wa Daftari.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano wa Tume na wadau wa uchaguzi uliofanyika mkoani Tabora tarehe 20 Novemba, 2023 Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Balozi Omar Ramadhan Mapuri amewapongeza wakazi wa mkoa huo kwa mkoa wao kuwa miongoni mwa mikoa miwili ambayo kata zake ziliteuliwa kufanya majaribio hayo ambayo yamefanyika kuanzia tarehe 24 hadi 30 Novemba, 2023.

Mhe. Mapuri amezitaja kata hizo kuwa ni kata ya Ng'ambo iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, ya mkoa wa Tabora na kata ya Ikoma iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, katika Mkoa wa Mara.

"Tume inawapongeza wakazi wa Mkoa wa Tabora kwa mkoa wenu kuteuliwa kuwa mwenyeji wa zoezi hili la uboreshaji wa

majaribio wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura," amesema Mhe. Mapuri.






# Wahimizwa kutoa taarifa za Wapiga Kura waliopoteza sifa

*Na Mwandishi wetu*

Wananchi wamehimizwa kutoa taarifa za wapiga kura waliopoteza sifa za kuwemo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili waweze kuondolewa katika zoezi la uboreshaji wa majaribio ambalo lilifanyika kuanzia tarehe 24 hadi 30 Novemba, 2023 katika kata ya Ng'ambo iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na Ikoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya.

Wito huo umetolewa tarehe 28 Novemba, 2023, na Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga Kura Bi. Giveness Aswile, mara baada ya kuvitembelea vituo mbalimbali vya kujiandikisha ambavyo vilitumika kwenye zoezi la uboreshaji wa majaribio katika kata ya Ng'ambo, iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Amefafanua kuwa kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa taarifa za watu waliofariki ambao kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wanatambulika kuwa ni watu waliopoteza sifa za kuwemo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, na hivyo majina yao yanapaswa kuondolewa kwenye Daftari hilo.

"Bado upatikanaji wa taarifa za

waliofariki japo kisheria tunasema watu waliopoteza sifa za kuendelea kuwemo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, namna ya upatikanaji wa taarifa zao ni changamoto kwa sababu hakuna mtu anayekuja kutoa taarifa hizo," amesema na kuongeza:

"Kuna kituo ambacho tumepita tumeona Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa ameorodhesha majina ya watu kumi na moja lakini ni mtu mmoja tu ambaye taarifa zake zimekamilika ina maana hao wengine itabidi Tume izitafute taarifa zao katika mfumo na kuzihakiki kama majina yaliyoorodheshwa ni ya hao wenyewe."

Ameongeza kuwa, suala la upatikanaji wa taarifa za wapiga kura waliopoteza sifa za kuendelea kuwemo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni miongoni mwa mambo ambayo Tume inapaswa kuendelea kuyafanyia kazi.

Amesema mafanikio ya zoezi la uboreshaji wa majaribio siyo kuwaandikisha na kuwapata wapiga kura wengi bali ni kuangalia mambo gani yanayowahusu wapiga kura ambayo Tume imeyaona kama changamoto katika zoezi hilo na inafanya nini ili kuyapatia ufumbuzi.

Aidha Mkurugenzi huyo wa Habari na Elimu ya Mpiga Kura amewapongeza wadau wa uchaguzi hasa wadau wakuu ambao ni

vyama vya siasa kwa kujitokeza kuunga mkono zoezi hili kwa kuweka mawakala ambao wamefanya kazi kubwa ya kuhamasisha watu kujitokeza kujiandikisha katika uboreshaji wa majaribio.

"Na hilo hasa ndiyo jukumu lao, tunatakiwa tushirikiane na hawa wenzetu wakihamasisha kwa sababu wale siyo wapiga kura wa Tume bali ni wapiga kura kwa ajili ya vyama vya siasa kwani wao ndiyo wenye wapiga kura, kwa hiyo nashukuru kwa vyama ambavyo vimeona umuhimu wa kushiriki katika hili zoezi," ameeleza Bi. Aswile

Pia Bi. Aswile amevishukuru vyombo vya habari kwa kuhabarisha umma juu ya nini kilikuwa kinaendelea katika kipindi chote cha zoezi la uboreshaji wa majaribio katika kata za Ng'ambo na Ikoma kwa sababu zoezi hilo litafanyika nchi nzima hivyo ni haki ya kila mtanzania kujua nini kilikuwa kinaendelea katika kata hizo mbili.




Tume ya Taifa ya Uchaguzi
Makao Makuu Dodoma,
5 Barabara ya Uchaguzi,
41107 Njedengwa,
Uchaguzi House,
Anuani: S.L.P 358, Dodoma
Namba ya simu: +255 26 2962345-8
Nukushi: +255 26 2962348
Barua pepe: Uchaguzi@nec.go.tz

www.nec.go.tz tumeyauchaguzi_tanzania

Tume ya Uchaguzi-TZ Tume ya Uchaguzi-tz NEC online TV